



AZIMIO NA. 5/2014

AZIMIO LA BUNGE LA KUFUTA AU KUSAMEHE MADAI NA HASARA ZITOKANAZO NA UPOTEVU WA FEDHA NA VIFAA VYA SERIKALI KWA KIPINDI KILICHOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2011

KWA KUWA, kwa mujibu wa Kifungu cha 5 cha Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348, Waziri wa Fedha amepewa mamlaka ya kusimamia na kudhibiti matumizi ya Fedha za Umma ikiwa ni pamoja na kugawa na kuidhinisha matumizi ya fedha hizo baada ya kupata idhini ya Bunge;

NA KWA KUWA, kwa mujibu wa Kifungu cha 43(1) cha Sheria ya Fedha za Umma, Bunge linaweza, kwa Azimio la Bunge, kutoa idhini kwa Waziri wa Fedha kufuta hasara na upotevu wa fedha na vifaa vya Serikali, madai ya kodi pamoja na riba itokanayo na malimbikizo ya kodi;

NA KWA KUWA, Vitabu vya Hesabu ya Serikali vimeonyesha kuwepo kwa upotevu wa fedha na vifaa vya Serikali pamoja na maduhuli yasiyoweza kukusanywa;

NA KWA KUWA, kutokana na upotevu na upungufu huo wa fedha, vifaa na maduhuli ya Serikali, upo umuhimu wa kusahihisha katika Vitabu vyatya Hesabu za Serikali kwa kusawazisha kumbukumbu;

HIVYO BASI, kwa mujibu wa Kifungu cha 43(1) cha Sheria ya Fedha za Umma, sasa Bunge hili, katika Mkutano wa Kumi na Sita na Kumi na Saba, linaazimia kuidhinisha Waziri wa Fedha asamehe na kufuta hasara na upotevu wa fedha, vifaa vyatya Serikali pamoja na maduhuli yasiyoweza kukusanywa ili kusawazisha kumbukumbu katika Vitabu vyatya Hesabu za Serikali kama ifuatavyo:-

- (a) Upotevu wa fedha na vifaa vyatya Serikali – **Shilingi 10,296,281,100.23**; na
- (b) Maduhuli yasiyoweza kukusanywa **Shilingi 519,824,082.39**
Jumla kuu ni **Shilingi 10,816,105,182.62**.

Limepitishwa na Bunge leo tarehe 17 Novemba, 2014.

Dkt. T. D. Kashililah
KATIBU WA BUNGE